

Masharti ya Matumizi

Wanafunzi/wazazi/walezi ni lazima wafuatilie Sera na Utaratibu unao husiana na matumizi ya teknolojia ya Wilaya na vifaa wakati wote ndani na nje ya Wilaya. Ukosefu wowote wakutofuatilia unaweza sababisha kitendo cha nidhamu na usitishaji wa haki za mmiliki za mwanafunzi kwa mali na rasilimali za kompyuta za Wilaya. Vifaa vyote na zanaa ni lazima zirudishwe zikiwa katika hali nzuri shuleni kabla ya siku ya mwisho ya kalenda ya mwaka wa shule, isipokuwa pale umiliki umesitishwa mapema na maofisa wa Wilaya au baada ya wanafunzi kujitoka kutoka shuleni.

Dhima

- 1 Mwalimu wa mwanafunzi au usimamizi wa shule unapaswa kuwasiliwa mara moja ikiwa mali imeharibiwa, imepotea au kuibiwa.
- 2 Ripoti ya polisi ni lazima iwekwe kwa faili na nakala ipeanwe katika shule yako ikiwa kutakuwa na uwizi, uharibifu au vitendo vingine vya uhalifu.
- 3 Mwanafunzi au familia ya mwanafunzi ita wajibika kwa gharama ya urekebishaji/ubadilishaji ikiwa:
 - a Uharibifu ni kwa ajili ya uzembe au tendo la kusudi.
 - b Kifaa kimepotea au kuibiwa kwa ajili ya uzembe au tendo la kusudi.
 - c Kifaa hakirudishwi Wilayani katika mwisho wa mwaka wa shule.

Ufuatiliaji na Usimamizi wa Kifaa

- 1 Vifaa vyote vya mkononi zita wekwa programu kuzi fuatilia endapo kutakuwa na hasara au uwizi. Programu hii ina uwezo wa kufuatilia mwendo na matumizi ndani na nje ya Wilaya
 - a Programu ya kufuatilia ita wezeshwa endapo kutakuwa na hasara au uwizi kwa kifaa au kusaidia wachunguzi kuhusiana na usalama wa mwanafunzi.
- 2 Vifaa vyote vya mkononi zinazotoka Wilayani ni lazima zijumuishe programu ya kuchuja tovuti. Programu hii inawekwa kuhakikisha usalama wa mwanafunzi.
 - a Programu ya kuchuja tovuti itakuwa na uwezo wa kufuatilia matumizi ya kifaa ndani na nje ya Wilaya.
 - b Majaribu ya kuzima au lemaza programu ya kuchuja tovuti ina kataliwa na itachukuliwa kama ukiukaji wa sera hii

Mwongozo wa Jumla wa Kifaa

- Wanafunzi hawana matarajio ya faragha. Wilaya inaweza kufuatilia taarifa yeyote iliyo hifadhiwa au kusafirishwa kupitia kifaa hicho.
- Vifaa vya mkononi vinavyo milikiwa na Wilaya zitapewa lebo ya idhini ya kukubaliwa ya wilaya. Lebo ni lazima isi tolewa kwa sababu yeyote.
- Wanafunzi wanapaswa kuarifu mwalimu wao au usimamizi wa shule endapo kifaa hakifanyi kazi vizuri.
- Faili/hati haziwezi kufutwa na mtu yeyote isipokuwa na mwenyewe/mmiliki asili.
- Yaliyomo yasiyofaa hayawezi kuhifadhiwa, kusafirishwa au kufikiwa katika vifaa vya Wilaya
- Wanafunzi ni lazima waingie wakitumia jina la matumizi na nywila walizopewa.
- Wanafunzi hawapaswi kugawa kwa watu wengine taarifa yao ya kuingia.
- Kila kifaa kina peanwa kwa mwanafunzi mmoja binafsi. Wanafunzi hawapaswi kamwe “kubadilishana” au “kugawa” kifaa chao na mwanafunzi mwingine.

- Vifaa vya mkononi ni lazima zirudishwe kwa Wafanyakazi wa Wilaya kwa urekebishaji ikiwa hazifanyi kazi vyema. Tafadhali usijaribu kurekebisha kifaa wewe mwenyewe. Jaribu lolote kwa urekebishaji wa kifaa kwa mtu asiye pewa idhini itasababisha mwanafunzi awajibike kwa gharama kamili ya ubadilishaji wa kifaa hicho.

Majukumu

Mwanafunzi

- Wanafunzi wanawajibika kila mara kwa kifaa chao, hata kama ni shuleni au nyumbani.
- Wanafunzi wana majukumu ya kuleta kifaa chao shuleni kila siku.
- Wanafunzi hawapaswi kukopesha kifaa chao au sehemu yeyote inayo husiana kwa mwanafunzi yeyote kwa sababu yoyote.
- Wanafunzi wana majukumu ya kuchaji na kuhifadhi betri ya kifaa chao kila siku.
- Wanafunzi wana majukumu ya kuhakiki na kufuatilia sera za Wilaya na za shule husika.

Mzazi

- Wazazi/walezi wana majukumu ya kufuatilia matumizi ya kifaa cha mtoto wao wakati wako nje ya maeneo ya Wilaya.
- Wazazi/walezi wana majukumu ya kuhakiki Sera ya Matumizi Yanayokubalika ya PPSD na mwanafunzi wao

Utaratibu wa Kurudi

Katika mwisho wa mwaka wa shule, au mapema kama itakavyo amuliwa na Wilaya, wanafunzi watarudisha kifaa na zanaa zake zote shuleni.

Vifaa na zanaa zita hesabiwa na kukaguliwa endapo zina uharibifu. Wanafunzi wata wajibika kwa sehemu zozote zinazo kosekana.